Jaribuni Hizo Roho

na

Ellis Forsman

Jaribuni Hizo Roho

na

Ellis Forsman

Oktoba 7, 2011

Jaribuni Hizo Roho

1 Yohana 4:1-6

Hapo awali katika waraka huu, Yohana amezungumzia jinsi ambavyo uhusiano wetu unavyopaswa kuwa (au haipaswi) kwa kuzingatia:

- Mungu – 1 Yoh. 1:5-6, *"Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lolote halimo ndani yake. Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli."*
- Yesu – 1 Yoh. 2:3-4, *"Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye, asema, nimemjua wala hazishiki amri zake, ni mwongo wala kweli haimo ndani yake."*
- Vitu vilivyoko duniani – 1 Yoh. 2:15, *"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake."*
- Dhambi- 1 Yoh. 3:4-5, *"Kila atendaye dhambi, afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi. Nanyi mnajua ya kuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake."*
- Ndugu zetu - 1 Yoh. 3:11, *"Maana hii ndiyo habari mliyoisikia tangu mwanzo, kwamba tupendane sisi kwa sisi."*

Sura ya nne inaanza na Yohana akiimiza kuhusu mabadiliko ay ohayo: manabii wa uongo!

1 Yohana 4:1-6, *"Wapenzi msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetoka kwa Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani. Katika hili mwamjua Roho wa Mungu, kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndiyo roho ya mpinga Kristo ambayo mmesikia kwamba yaja; na sasa imekwisha kuwako duniani. Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia."*

Kwa maneno mengine ya upendo (*"wapendwa"*), alafu, Yohana anawahimiza ndugu zake ili…

Jaribu Roho!

Msiamini kila roho.

1 Yoh. 4:1, *"Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani."*

Usiamini kilakitu unacho sikia, au kila mtu anaye dai kuwa ametoka kwa Mungu. Utakuwa ni ujinga wa namna gani kwa kufanya hivyo, ni kawaida.....

Tutakuwa katika hali iliyokithiri ya kuchanganyikiwa (amini kitu kimoja wakati mmoja, na kitu kingine wakati mwingine). Tutakuwa rahisi kuongozwa vibaya na wale wanaofundisha uongo.

Zijaribuni roho.

1 Yoh. 4:1, *"Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.*

Neno "*jaribu"* ("jaribu"- katika Biblia ya NIV) inamanisha....

- Kuchunguza, Kuthibitisha (Thayer).
- Kuona kitu kama ni halisi au hapana.

Kwa hiyo usikubali kile ambacho baadhi ya waalimu au wahubiri wanasema; chunguza kile kilichofundishwa. Wale walio na tabia kama hii wameonywa sana kwa hali ya juu katika maandiko.

- **Waberoya** – Matend. 17:11, *"Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo."*
- **Waefeso** – Ufu. 2:2, *"Nayajua matendo yako na taabu yako, na subira yako, nayakuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya, tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio ukawaona kuwa waongo."*

Kwa sababu ya manabii wa uongo.

1 Yoh. 4:1, *"Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani."*

Hii ndiyo sababu ya *"kuzi jaribu roho"*

Wengine nao wametuonya juu ya ukweli huu...

- **Yesu** – Math. 7:15, *"Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali."*
- **Petro** – 2 Pet. 2: 1- 3, *"Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakapo ingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia. Na wengi watafuata ufisadi wao; na kwa hao njia ya kweli itatukanwa. Na katika kutamani watajipatia faida kwenu na maneno yaliyotungwa; ambayo hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii."*
- **Paulo** – 2 Wakor. 11: 13-15, *"Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu maana shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao."*

Kwa hiyo ni lazima tuchunguze, tuhakikishe, tuthibitishe kila kitu ambacho kinafundishwa! Lakini KIVIPI tunavyoweza kuzijaribu roho? Katika kifungu chetu cha maandiko, Yohana anashirikiana nasi majaribio kadhaa.....

Majaribio

Je wanakiri kwamba Yesu amekuja katika mwili?

- 1 Yoh. 4:2-3, *"Katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila Roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila Roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndiyo roho ya mpinga Kristo ambayo mmesikia kwamba yaja; na sasa imekwisha kuwako duniani."*
- 1 Yoh. 4:6, *"Sisi twatokana na Mungu. Yeye amjuaye Mungu atusikia; yeye asiyetokana na Mungu hatusikii. Katika hili twamjua Roho wa kweli, na roho ya upotevu."*

Mistari hii 2-3 yameeleweka vizuri sana kwa upande wa wale waliofundisha uongo ambao walikuwa wengi kwa kipindi kile ambao wengine walimkana Yesu Kristo kwa hajaja katika mwili.

2 Yoh. 1:7, *"Kwa maana wadanganyifu wengi wametokea katika dunia, ambao hawamkiri Yesu Kristo kwamba amekuja katika mwili. Huyo ndiye yule mdanganyifu na mpinga Kristo."*

Ambao mafundisho yao yalikuwa yanawapotosha watu, ikiwezekana kwa sababu waalimu wa uongo wanadai kwamba wamevuviwa na roho.

Lakini wale watakaofundisha upotovu huo hawaongozwi na Roho wa Mungu, bali wanakuwa na roho ya mpinga Kristo!

2 Yoh. 1:7, *"Kwa maana wadanganyifu wengi wametokea duniani, wasiokiri ya kwamba Yesu Kristo yuaja katika mwili. Huyo ndiye yule mdanganyifu na mpinga Kristo.*

Je wanawasikiliza mitume wa Kristo?

1 Yoh. 4:6, *"Sisi twatokana na Mungu. Yeye amjuaye Mungu atusikia; yeye asiyetokana na Mungu hatusikii. Katika hili twamjua Roho wa kweli, na roho ya upotevu."*

Kifungu hiki kinafunua jinsi tunavyoweza kutofautisha "roho wa kweli" na "roho wa uongo"

- Wale ambao kweli wanamjua Mungu wanawasikia mitume.
- Wale ambao si wa Mungu atawakataa.

Je mafundisho yanakubaliana na kile ambacho mitume walifundisha? Kwa sababu Yesu alifundisha kwamba kuwapokea ni kumpokea yeye na Mungu.

Yoh. 13: 20, *"Amin, amin, nawambieni, yeye ampokeaye mtu yeyote nimpelekaye, anipokea mimi; naye anipoakeye mimi; ampokea yeye aliyenipeleka."*

Hivyo, kanisa la kwanza liliendelea kudumu katika fundisho la mitume.

Matend. 2:42, *"Na wakaendelea kudumu katika fundisho la mitume na katika ibada, katika ushirika na katika kumega mkate na katika kusali."*

Walitambua maneno yao kama maagizo kutoka kwa Bwana.

1 Wakor. 14:37, *"Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo, ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*

Hata mitume waliwatambua mitume wengine wakiandika maneno yaliovuviwa.

2 Petr. 3:15-16, *"Nanyi uhesabuni uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu, kama vile na ndugu yetu mpenzi Paulo alivyowaandikia kwa hekima aliyopewa; vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio*

imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na maandiko mwngine, kwa uvunjifu wao wenyewe."

Kwahiyo, wale walio wa Mungu watawasikiliza mitume, na kukubali mafundisho yao!

Hili ndilo jaribio ambalo tunaweza kwa urahisi kulitumia leo katika kila mambo!

Lakini inaonyesha hekima na uelewa wa mafundisho ya mitume katika upande wetu. Hivyo, hiyo haiwezi kuwa tatizo kama tukifuata mifano ya kanisa la kwanza la Yerusalemu.

Matendo. 2: 42, *"Wakaendelea kudumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kumega mkate, na katika kusali."*

Hatakama haijaonyeshwa na Yohana, hapa kuna "*majaribio"* mawili zaidi:

Jaribio la Kumbukumbu 18:21-22, *"Nawe ukisema moyoni mwako, tutajuaje neno asilolinena BWANA? Atakaponena nabii kwa jina la BWANA, lisifuate jambo lile wala kutimia, hilo ndilo neno asilolinena BWANA, kwa kujikinai amelinena huyo nabii, usimwogope."*

Ikishatumika mtu akidai ya kuwa ni nabii wa Mungu. Kama unabii wao ukishindwa, wanasemwa kuwa ni manabii wa uongo.

Jaribio la Kumbukumbu. 13: 1-4, *"Kukizuka katikati yako nabii au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au ajabu, ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akisema, na tuifuate miungu mingine usiyoijua, tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii Yule, au Yule mwotaji wa ndoto, kwa kuwa BWANA Mungu wenu yuawajaribu, apate kujua kwamba mwampenda BWANA, Mungu wenu kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote. Tembeeni kwa kumfuata BWANA, Mungu wenu mcheni na kushika maagizo yake, na kuisikia sauti yake, nanyi mtumikieni na kushikamana naye."*

Kutumika wakati maajabu yanafanywa, na unabii unaonekana kwamba unatimia. Kama mafundisho yao yana pingana na kile Mungu amekifunua tayari, lazima wakataliwe (hiki ndicho sawasawa na kile Yohana alikiandika).

Hitimisho

Katikati ya haya maonyo "*Kujaribu roho"*, Yohana anatoa maneno ya faraja katika mistari ya 4 -5:

1 Yoh. 4: 4-5, *"Ninyi watoto wadogo, mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia. Hao ni wa dunia; kwa hiyo wanena ya dunia na dunia huwasikia."*

Kwa kuwa wa Mungu (kwa sababu wamesikiliza maneno ya mitume wake), wanaweza kuwashinda manabii wa uongo, kwa sababu Mmoja kati yao ni mkuu kuliko (Shetani?) ambaye yupo katika ulimwengu.

Usishangae kuona dunia inafuata manabii wa uongo, kwa sababu manabii wa uongo ni wa dunia na wanaongea yaliyoko duniani; kwa hiyo usisumbuke na "mafanikio" ya waalimu wa uongo (idadi na kiwango siyo vipimo sahihi vya ukweli!).

Kwa mtazamo wa wingi wa dini na mafundisho mengi yanayotuhimiza sasa, yote ni kwa jina la Kristo na Roho wa Mungu, kuhimiza kwa Yohana ni ya wazi na ni muhimu kwetu sisi:

1 Yoh. 4:1, *"Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho kwamba zimetokana na Mungu, kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani."*

Je unaendelea kudumu katika mafundisho ya mitume ili kwamba uweze kutumia jaribio kwa usahihi?